**African Entrepreneurs – Successful and Responsible**

**EPISODE 02**

**TITLE: The Kenyan Toilet Revolution – David Kuria**

**Author: Eric Ponda**

**Editors: Katrin Ogunsade, Adrian Kriesch**

**Proofreading: Natalie Glanville-Wallis**

**Kisuaheli: Eric Ponda**

## Characters (O-Töne, Clips) / Narrators

| | Women | Men | Age | Language |
|---|---|---|---|---|
| Intro/Outro | X | | Unimportant | |
| Narrator | | x | Unimportant | |
| David Kuria (clip) | | x | 30s | English |
| Customer 1 (clip) | | x | 40s | English |
| Customer 2 (clip) | | x | 30s | English |
| Gladys | X | | 30s | English |

**INTRO….**

Hujambo na kwa mara nyingine karibu katika mfululizo wa mchezo mwengine wa vipindi vya Learning By Ear, Noa Bongo Jenga Maisha yako. Katika mfululizo wa vipindi hivi tunawaangazia Wajasirimali wanotajika Barani Afrika na wanaochangia pakubwa katika maendeleo ya jamii wanamoishi .

Katika makala ya leo tunafunga safari hadi Mji mkuu wa Nairobi nchini Kenya ambako tunakutana na Mjasirimali mmoja anayebadilisha maisha ya wengi kutokana na uvumbuzi wake wa ujenzi wa Vyoo vya umma vinavyozingatia usafi wa hali ya juu na pia mazingira

**1. SFX: Noise on the road, Car hooting, Touts calling passengers from a distance.**

## 2. Narration

Ni saa kumi na moja alfajiri na tayari David Kuria yumo mbioni Barabarani kufanya kazi anayoipenda zaidi. Amemaliza kukagua Choo kilichojenga katika kituo cha Mabasi kati kati mwa jiji la Nairobi. Na bado kuna vyoo kadhaa vinavyosubiri kukaguliwa kabla ya saa mbili asubuhi, anapohitajika kuwa ofisini mwake umbali wa kilomita 8 nje kidogo tu kutoka kati kati mwa Jiji la Nairobi. Ni mapema sana na kibaridi cha asubuhi bado kinavuma, lakini kwa David hii si hoja il mradi atimize wajibu wake wa kuhakikisha vyoo vyote ni Safi kabla ya msongamano wa wateja. Kazi inayomfanya atambulikane miongoni mwa wakaazi wa jijini hili. Vyoo hivyo vyenye mwangaza wa kutosha, na ambavyo vinadumisha usafi wa hali ya juu hutoa huduma kwa masaa 24 kwa siku huku wafanyi kazi wakipokezana kwa zamu.Davidi ambaye amesomea taaluma ya usanifu Mjengo sasa ameelekeza juhudi zake katika kazi hii kwa muda wa miaka 3 iliyopita. Yenye ndie muasisi wa Kampeini ya kuboresha usafi wa Vyoo Barani Africa inayofahamika kama IKO TOILET.

**3. OTON 1 David Kuria**

"Nimekuwa nikijishughulisha na miradi ya kuboresha maendeleo ya miji katika kanda ya Afrika Mashariki kwa muda wa miaka 13 iliyopita, na hapo ndipo wazo mradi huu wa IKO TOILET liliponikujia miaka mitatu iliyopita.Ukweli ni kwamba suala la usafi wa umma limepuuzwa karibu sehemu zote kote nchini. Ndio sababu ugonjwa wa Malaria huzuka takriban kila mwaka katika mataifa ya kanada hii. Na miji yetu ikianza kukumbwa na maradhi haya, ni dhihirisho kwamba kiwango cha usafi wa mazingira yetu ni cha kusikitisha."

4. **Narration:**

David Kuria ni muasisi wa mpango wa ujenzi wa vyoo vya umma ambao umefaulu sana, katika juhudi za kuboresha usafi wa mitaa mingi ya mabanda na isiyo muundo mbinu bora nchini Kenya.Chini ya shirika kale la ECOTACT, David anaihusisha jamii moja kwa moja katika kupanga na kujenga vyoo hivi vinavyofahamika sana kama IKO Toilets, ambavyo sio tu ni muhimu kwa wakaazi wa jiji la Nairobi kwa huduma zake bali pia kuwa sehemu muhimu za kibiashara.

**5. OTON 2 David Kuria (eng)**

"Tangu tupate uhuru wetu miaka 40 iliyopita, kumekuwa na hali ya kukata tama miongoni mwa Wakenya wengi hasa katika utoaji wa huduma hizi kutokana na kuongezeka kwa idadi ya watu.Mabaraza ya miji yamejikuta katika njia panda na kushinda jinsi ya kushughulikia suala hili. Kumekuwa na msukumo kutoka kwa wananchi wa kuboreshwa kwa huduma hizi za usafi wa vyoo vya umma katika sehemu za miji.Kwa hiyo tunachofanya si kujitwika jukumu la serikali utoaji wa huduma hizi bali ni kuichochea serikali kuimarisha huduma hizi. Kwa hivyo, uvumbuzi wetu au mradi huu ni kuonyesha umma kwamba yawezekana.!

**6. Narration:**

Mradi huu umebadilisha sura ya sehemu nyingi za miji na mitaa ya mabanda hasa katika mtaa wa mabanda wa Kibera jijini Nairobi unaosemekana ndio mkubwa zaidi barani, ambako waakaazi wake wanarusha kinyesi kupitia dirishani. Hapa wakaazi hujisaidia kwenye mifuko ya plastiki na kisha kutupa kinyesi hicho kupitia dirishani bila ya kujali utakakoanguka mfuko huo wa kinyesi.

Wakaazi wengi wa Nairobi waliona aibu kwenda katika choo cha Umma kujisaidia, lakini wazo la David Kuria kuanzisha na kuboresha usafi wa vyoo vya umma jijini, kumeondolea mbali kasumba hii na sasa vyoo hivi vinawavutia wateja wengi sana. Tunakutana na mmoja wao katika choo hiki cha IKO kati kati mwa jiji la Nairobi.

**7. SFX. : Business environment, people chatting, banging of steel doors**

**8. Oton 3 Costumer (eng)**

"Tangu mradi huu uanzishwe, vyoo vya Iko, vimebadilisha maisha ya wengi kutokana na huduma zake za hali ya juu, usafi na hata huduma nyingine za biashara kama vile kutuma  na kupokea pesa kwa kutumia simu ya mkononi.Sioni gharama kulipa ada ya shilingi 10 sawa na senti kumi za Euro. Ni sawa kabisa kulipa ada hiyo, kwani najisikia nyumbani kabisa kutumia huduma hizi. Isitoshe mradi huu umepunguza ile harufu mbaya ambayo ilikuwa jambo la kawaida jijini. Sasa sioni tena aibu kutumia choo cha umma!"

**9. Narration:**

Usafi wa vyoo si jambo linalojadiliwa wazi wazi, na ni mwiko katika mataifa mengi barani Afrika. Lakini mradi huu wa IKO umebadilisha kabisa dhana hii, na kutoa ajira kwa vijana wengi. Mbali na hayo, mradi huu wa IKO umesaidia kupanua biashara kwa wajasirimali wengi kupitia mpango wa kutoa haki za umiliki wa vyoo hivi.Hii ni kusema kwamba si kila mahali David anatekelezi mradi huu yeye binafsi bali kutoa haki za umiliki kwa waekezaji wengine ambao hujenga na kusimamia vyoo hivyo kwa niaba ya kampuni yake ya ECOTACT.

Mradi huu ulianzishwa kwa ufadhili wa makundi ya vijana na misaada kutoka kwa mashirika ya kitaifa na kimataifa.

Lakini baadaye, ukaimarika na kuanza kuleta mapato kutokana na ada inayotozwa wateja wanaotumia huduma hizi, matangazo ya biashara ya kampuni mbali mbali kama vile kampuni zinazotoa huduma za simu na kadhalika. Pia hukusanya pato kwa kukodisha sehemu za majengo hayo ya vyoo kwa wafanyi biashara wadogo wadogo kama vile wapigaji rangi viatu.

**10. OTON 4 David Kuria**

"Mradi huu umebuni nafasi nyingi za kazi. Mfano ukienda katika choo nyingi za IKO, ambazo sasa zinafahamika kama kumbi za biashara kutokana na shughuli nyingi, utakutana na vijana wengi wakifanya kazi za kung'arisha viatu. Kazi za aina hii mara nyingi hufanywa na vijana kwa wasichana kutoka mitaa ya mabanda.Kwa hiyo choo hizi sio tu zinatoa huduma za usafi bali pia kujaribu kubadilisha fikra za watu kuhusu suala la usafi wa vyoo vya umma. Wazo hili pia limepanua fikra za biashara kama vile *'kuchaji simu'* yaani kuweka nguvu za umeme kwenye simu za mkononi,kung'arisha viatu, na kadhalika, ambapo sasa tunasema,hatuendi chooni bali kumbi za biashara' Watu sasa wanapiga foleni kung'arishiwa viatu…wapi? Katika choo za Ikotoilet…! Ama kwa hakika utapata huduma zote hapa katika vyoo hivi ambavyo naweza kusema ni duka kubwa la usafi."

**11. Narration:**

Kama ilivyo katika mataifa mengi barani Africa, ukosefu wa ajira ni tatizo kubwa nchini Kenya, na hivyo vijana wengi husalia tu kuihangaika huku na kule kutafuta kazi za ofisini. Lakini sasa mradi huu huenda utaleta afueni kubwa kwa wakazi wengi wa jiji kama mkaazi mmoja,ambaye ni mteja katika vyoo hivi anavyosema.

**12. Oton 5 Costumer 2 (eng).**

"Tunalipa kodi kubwa sana kwa serikali, lakini hatupati huduma muhimu na bora kama choo safi zenye mazingira bora kama hivi vya Iko. Hebu fikiria nafasi za kazi zinazobuniwa kwa Wakenya kupitia mradi huu wa IKO. Je kama mradi huu ungetekelezwa katika miji yote mikubwa nchini, unadhani ni Wakenya wangapi wataajiriwa?"

**13 Narration**

Lakini safari ya Davidi haikuwa rahisi kufika mahali alipo sasa. Kinachompa msukumo zaidi David ni subira ambayo si wengi waliyonayo hasa miongoni mwa vijana wengi, anasema. Ilimchukua muda wa miaka kumi kuwashawishi maafisa wa serikali ya Kenya kulikubali wazo lake la kuanzisha mradi huu.

**14 OTON 6 David Kuria (Eng)**

"Watu wengi niliozungumza nao kuhusu mradi huu waliniambia unapoteza wakati wako bure kuanzisha mradi ambalo hauwezi kufaulu! Wewe ni Mtu aliyesoma na mwenye taaluma ya usanifu mijengo, kwanini usitafute kazi ufanya badala ya kupoteza muda wako! Ilinichukua takriban muda wa mwaka mmoja kushauriana na maafisa wa serikali… Sasa haya ndio mambo ambayo vijana wengi wanashindwa kuvumilia… Miaka kumi iliyopia, ni wachache sasa wangekubali kufanya kazi katika Vyoo vya umma.Lakini sasa watu wanatuma maombi ya kutaka kuajiriwa… Kunao wenye stashahada yaani Diploma na wanatuma maombi kutafutakazi katika Vyoo vya IKO. Siku hizi kufanya kazi katika vyoo hivi imekua kazi ya kawaida inayoheshimiwa pia. Lengo letu kubwa tulitaka kubadilisha mtazamo na kuimarisha huduma hizi…! Kwani siku hizi kufanya kazi katika choo cha Iko si kama kufanya kazi katika choo za kawaida za umma."

**15 NARRATION:**

Gladys, ni mmoja wa wahudumu katika choo hivi na anakubaliana na David.

**16 SFX Noise of cleaning up a Toilet,**

**17 Oton 7 Gladys Toilet Attendant (*Eng)***

"Mimi hufanya kazi kwa masaa 8.Kufanya kazi hapa si kama kufanya kazi katika choo nyingine zinazosimamiwa na mabara ya miji. Hapa hatufanyi kazi kupita kiasi isipokuwa tu wakati kuna uhaba wa maji. Hapa tunatoa huduma za aina mbali mbali.Unaweza kutuma pesa kwa jamaa zako ukiwa hapa chooni…! Hebu fikiria! Ni zaidi tunalipwa mshahara mzuri sana!"

**18 Narration:**

Wakati alipoanzisha shirika lake la ECOTACT miaka mitatu iliyopita, lengo kubwa la David lilikuwa kubadilisha mtazamo wa hali ya usafi wa choo za umma na kudumisha hali hiyo katika muktadha wa Kiafrica. Na sasa mtazamo au mfumo huu umeanza kutumika katika utoaji wa huduma nyingine za jamii kama vile usimamizi wa huduma za maji nchini Kenya.

**19 Oton 8 David Kuria (Eng)**

"Mbali na kuoboresha huduma za choo za Umma pia tunamipango ya kusimamia huduma za usambazaji maji kupitia mpango huu wa IKO n ifikapo kati kati mwa mwaka huu. Tutatumia mfumo huu kuchimba visima kote nchini Kenya na kujenga vituo vya maji kisha kuwakabidhi watu binafsi usimamizi wa huduma hizo. Na kwa kufanya hivyo tutaongeza nafasi za kazi kwa vijana.".

**20 Narration:**

Mtindi wa choo hizi sasa umeanza kukumbatiwa katika mataifa mengi yaliyoko kusini mwa jangwa la sahara,Na ndoto kubwa ya David ni kupanua huduma hizi katika shule zote za umma nchini Kenya huku mipango ikipiga hatua kusambaza mtindo huu hadi nchi jirani kama vile Tanzania, ambako tayari shirika la ECOTACT linashirikianiana na Baraza la Jiji la Dar es Salaam kutoa huduma hizi bora.

Licha ya juhudi hizi, David bado haridhiki na jinsi mambo yanavyokwenda. Sikitiko kubwa ni jinsi Watu wanavyolichukulia vivi hivi suala la usafi na ambapo wamekataa kubadilisha tabia ya kupuuza masuala ya kudumisha usafi.

**21 OTON 10 David Kuria**

“Kulingana na ripoti ya Umoja wa Mataifa, ni asilia mia 3 tu ya wanafunzi ambao wanazingatia mambo madogo madogo kama mazoea ya kunawa mikono, sasa fikiria asilimia 97 hawana habari kuhusu umuhimu wa kunawa mikono, jambo la kusikitisha sana. Tunawapa wateja wetu sabuni na maji katika choo hizi za IKO, lakini cha kushangaza ni kwamba utakuta watu wakiondoka chooni bila ya kuosha mikono licha ya kwamba amelipia huduma hizi. Ana sahau kuwa ametoka chooni kitu cha kwanza ni kununua chakula na kuanza kula au hata kukusalimia barabarani bila ya kuosha mikono… na ametoka chooni….! Hii inaonyesha wazi jinsi kiwango cha kudumisha usafi kilivyo chini miongoni mwetu..!

**22 NARRATION**

Huduma za vyoo vya IKO zimeleta mabadiliko makubwa katika jamii ambapo, zaidi ya watu milioni walitumia huduma hizi mnamo mwaka wa 2010. Hata hivyo lakini kama ilivyo kawaida, kila biashara inachangamoto zake hasa ikiwa Mtu hana ujuzi unaohitajika kusimamia biashara hiyo. Je suala hili linamtatiza David?

**23 OTON 11 David Kuria (eng)**

"Nadhani yote inategemea jinsi unavyotekeleza wazo lako kwa kuzingatia misingi ya utalaam, na ndio sababu hapa nina watalam 12 ambao wamehitimu katika taaluma mbali mbali.Jukumu langu ni kujenga msingi wa wafanyi kazi ambao wanauzoefu na kuleta pamoja fikra na taaluma zao kwa manufaa ya kuendeleza biashara hii.Na hivyo ndivyo ynavyoweza kujenga nidhamu ya kazi. Hapa tunawatalam wa masuala ya biashara,wahandisi, mauala ya jamii, na sote tuaangalia ni vipi tunapanua huduma au mradi huu kwa manufaa ya jamii!"

**24 NARRATION**

Kusimamia mradi kama huu wa IKO unahitaji kujitolea anasema David. Lakini je, biashara hii imebadilisha maisha yake ya kawaida? Anasema kuna wakati wa kila kitu, kuna muda wa kukaa na familia, na pia hutenga muda wa kupumzika. Anaitazama biashara hii kama lenye kutimiza ndoto ya maisha licha ya changamoto ambazo kawaida huwakumba wajasirimali chipukizi.

**25 OTON 12 David Kuria (Eng)**

"Mara nyingi utanikuta mimi na wafanyi kazi wengine tukifanya kazi hii ambayo wamekuja kuipenda hadi mwendo wa saa mbili usiku.Hebu tazama nafazi za ajira zilizopo katika sekta hii sasa. Tumewajiri vijana wengi sana. Na miaka kumi iliyopita hakuna Mtu angeweza kufikiria hivyo! Na hata kama ungekuwa na wazo hilo, watu wangekupuuza kwamba haliwezi kufauli hapa Barani Africa, pengine ukaanzishe mradi huo nchini Marekani au barani Ulaya."

**OUTRO:**

Na kwa maneno hayo kutoka kwa David Kuria muasisi wa choo za IKOTOILETS, ndipo tunafika mwisho wa kipindi cha leo kuhusu Wajasirimali chipukizi barani Afrika. Mwandishi wa makala haya ni Eric Ponda, tunakushukuru kwa kutusikiliza na iwapo unataka kufahamu mengi zaidi kuhusu kipindi himki au vingine vya Noa Bongo jenga Maisha yako, tembelea mtandao wetu wa www.dw.de/lbe. Hadi wakati mwengine kwa makala nyingine kwaheri kwa sasa.